JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# RIPOTI YA TATHMINI YA UTENDAJI YA MWAKA WA FEDHA 2016/17

TOLEO LA WANANCHI


Septemba, 2017

# YALIYOMO

UJUMBE WA MWENYEKITI WA BODI YA WAKURUGENZI ........ iii
UJUMBE WA MTENDAJI MKUU ........ iv
SURA YA KWANZA ........ 1
1.0 Utangulizi ........ 1
1.1 Malengo na majukumu ya PPRA ........ 1
1.2 Dhima na Dira ya PPRA ........ 1
1.3 Utekelezaji wa mpango mkakati ........ 2
SURA YA PILI ........ 3
2.0 Matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya PPRA ........ 3
2.1 Utendaji kwenye manunuzi ya umma ........ 3
2.1.1 Uwasilishaji wa taarifa za manunuzi ........ 3
2.1.2 Ushirikiano na taasisi nyingine ........ 4
2.1.3 Kufungia wazabuni kushiriki kwenye zabuni za umma ........ 5
2.1.4 Utoaji wa elimu ........ 5
2.1.5 Huduma za ushauri ........ 7
2.1.6 Mfumo wa uwasilishaji na upokeaji taarifa kwa njia ya kielektroniki ........ 7
2.1.7 Tovuti ya PPRA ........ 7
2.1.8 Jukwaa la majadiliano mtandaoni ........ 7
2.1.9 Huduma ya ujumbe mfupi wa simu ........ 7
2.1.10 Mfumo wa manunuzi kwa njia ya mtandao ........ 8
2.2 PPRA katika kufikisha huduma kwa wadau ........ 8
2.3 Kuboresha mazingira ya kazi na maslahi ya watumishi wa PPRA ........ 9
SURA YA TATU ........ 10
3.0 Ukaguzi wa manunuzi ya umma ........ 10
3.2.2 Mgawanyiko wa jumla ya thamani ya mikataba ........ 11
3.2.3 Thamani ya mikataba kulingana na makundi ya taasisi ........ 12
3.3.1 Malengo ya ukaguzi ........ 12
3.3.2 Uchaguzi wa taasisi na maeneo ya ukaguzi ........ 13
3.3.3 Aina za ukaguzi zilizofanywa ........ 13
*3.3.4 Matokeo ya ukaguzi wa uzingatiaji wa sheria* ........ 15

3.3.5 Matokeo ya ukaguzi wa kupima thamani ya fedha ... 16
3.5 Uchunguzi wa ukiukwaji wa sheria ... 18
SURA YA NNE ... 19
4.0 Changamoto na ufumbuzi wake ... 19
4.1 Changamoto ... 19
4.1.1 Changamoto za kisekta ... 19
4.1.2 Changamoto za ndani ya PPRA ... 20
4.1.3 Ufumbuzi ... 20

## UJUMBE WA MWENYEKITI WA BODI YA WAKURUGENZI



PPRA imekuwa ikiandaa ripoti ya tathmini ya utendaji kazi kuanzia mwaka wa fedha 2006/07. Lengo la ripoti hiyo, ambayo hutolewa kila mwaka, ni kuwafahamisha wadau namna PPRA inavyotekeleza majukumu yake na jinsi taasisi za Serikali zinavyozingatia sheria ya manunuzi.


Hata hivyo, PPRA imekuwa ikipokea maoni mbalimbali kutoka kwa wadau wake kuwa ripoti hiyo imekuwa ikiandaliwa kwa kutumia lugha ya kitaalam ambayo ni ngumu kueleweka kwa wananchi wa kawaida.

Ni kwa sababu hiyo na katika kutekeleza dhana ya utawala bora, mwaka 2016, PPRA ilianza kuandaa kijitabu hiki maalum kwa lugha rahisi ili kuongeza uelewa wa masuala ya manunuzi.

Aidha, kijitabu hiki husaidia kutoa mafunzo kwa jamii katika kufuatilia uwajibikaji wa taasisi za Serikali katika kutekeleza miradi mbalimbali.

Kama inavyofahamika, sehemu kubwa ya bajeti ya Serikali hutumika kwenye manunuzi. Hivyo, uelewa na ushiriki wa wadau wote, wakiwemo wananchi wa kawaida katika eneo hili, ni muhimu ili waweze kufuatilia matumizi ya fedha za umma katika manunuzi.

Ni matumaini yangu kuwa taasisi za Serikali, asasi za kijamii, wananchi na wadau wa manunuzi watakitumia kijitabu hiki kuongeza uelewa wa masuala ya manunuzi ya umma. Aidha, natarajia kitasaidia kuongeza uwazi, uwajibikaji na hamasa kwa wadau kwenye utekelezaji na ufuatiliaji wa miradi katika maeneo yao ili kupata huduma iliyokusudiwa.



Balozi Dkt. Matern Y. C. Lumbanga
**MWENYEKITI WA BODI**

## UJUMBE WA MTENDAJI MKUU



Kijitabu hiki kinahusu tathmini ya utendaji kazi wa PPRA kwa mwaka wa fedha 2016/17. Pamoja na mambo mengine, kinaonesha tathmini ya miradi, utoaji wa nyenzo mbalimbali na huduma za ushauri, mikakati ya mafunzo kwa wadau, na viwango vya uzingatiaji wa sheria, kanuni na taratibu za manunuzi ya umma.

Napenda kutumia fursa hii kuishukuru Serikali kwa kugharamia uchapishaji wa kijitabu hiki. Pia, naishukuru Bodi ya Uhariri ya *Tanzania Procurement Journal,* kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kuandaa kijitabu hiki.

Mwisho, napenda kuishukuru Bodi ya Wakurugenzi, menejimenti na watumishi wote wa PPRA kwa kufanikisha kazi hii.



Dkt. Laurent M. Shirima
**AFISA MTENDAJI MKUU**

## SURA YA KWANZA

### 1.0 Utangulizi

Ili Serikali iweze kutimiza mahitaji ya wananchi wake, ni lazima ifanye manunuzi mbalimbali yakiwemo ya vifaa, kazi za ujenzi au huduma kwa kutumia fedha zilizotengwa kwenye bajeti yake. Kwa mujibu wa sheria ya manunuzi ya umma, taasisi za Serikali hutakiwa kuandaa mpango wa mwaka wa manunuzi, sambamba na maandalizi ya bajeti. Aidha, sheria ya manunuzi imeweka misingi ya uwazi, ushindani na haki, inayopaswa kuzingatiwa na taasisi za Serikali ili kupata huduma bora.

Hivyo, ni jukumu la PPRA kusimamia manunuzi ya umma ili kuona kama misingi hiyo inazingatiwa katika utekelezaji wa miradi na utoaji wa huduma mbalimbali kama vile barabara, zahanati, shule, pembejeo, n.k.

Kijitabu hiki kinajumuisha maelezo ya namna PPRA ilivyotimiza wajibu wake wa kutunza taarifa za manunuzi na kutoa mafunzo ya manunuzi kwa wadau. Kitabu hiki pia kinaeleza namna taasisi za Serikali zilivyotimiza jukumu la kuwasilisha taarifa zao za manunuzi PPRA, na matokeo ya ukaguzi wa manunuzi uliofanywa kwa mwaka wa fedha 2016/17.

Sura ya Kwanza inatoa muhtasari wa malengo na majukumu ya PPRA na Sura ya Pili inaeleza utekelezaji wa majukumu yake.

Sura ya Tatu inahusu matokeo ya ukaguzi na uchunguzi kuhusiana na utendaji wa taasisi za Serikali katika manunuzi kwa mwaka wa fedha 2016/17.

Sura ya Nne na ya mwisho inahusu changamoto ambazo PPRA ilikabiliana nazo katika utekelezaji wa majukumu yake; pamoja na mikakati iliyojiwekea ili kuzipatia ufumbuzi na kuongeza ufanisi katika utendaji.

### 1.1 Malengo na majukumu ya PPRA

PPRA imeundwa chini ya sheria ya manunuzi ya umma na imepewa uwezo na jukumu la kusimamia na kudhibiti manunuzi ya umma nchini. Miongoni mwa majukumu ya PPRA ni kufuatilia uzingatiaji wa sheria ya manunuzi ya umma na kufanya uchunguzi kuhusu ukiukwaji wa sheria hiyo.

### 1.2 Dhima na Dira ya PPRA

**Dhima**
Kusimamia na kudhibiti mfumo wa manunuzi ya umma ili kuleta thamani bora ya fedha kwa maendeleo ya Taifa

**Dira**
Mfumo wa manunuzi ya umma unaozingatia uadilifu na unaohakikisha thamani bora ya fedha

### 1.3 Utekelezaji wa mpango mkakati

PPRA ilianza utekelezaji wa majukumu yake kwa kutumia mpango mkakati wa awamu ya pili Julai 2015, ukiwa na malengo makuu yafuatayo:

i) Kuboresha utendaji kwenye manunuzi ya umma;
ii) Kuimarisha uwezo wa PPRA katika kufikisha huduma kwa wadau; na
iii) Kuboresha mazingira ya kazi na maslahi ya watumishi.

# SURA YA PILI

## 2.0 Matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya PPRA

Yafuatayo ni matokeo ya kazi zilizofanywa na PPRA katika mwaka wa fedha 2016/17:

## 2.1 Utendaji kwenye manunuzi ya umma

Katika eneo hili, PPRA ilifanya ukaguzi wa manunuzi kwa taasisi za Serikali kama inavyooneshwa kwenye Sura ya Tatu. Pamoja na kufanya ukaguzi wa kawaida, PPRA pia ilifanya uchunguzi kwenye manunuzi.

### 2.1.1 Uwasilishaji wa taarifa za manunuzi

PPRA ina mfumo wa ufuatiliaji michakato ya manunuzi ambao unahitaji taasisi za serikali kuwasilisha taarifa za mipango ya manunuzi na baadaye ripoti za utekelezaji wake ili kuongeza uwazi.

Katika mwaka wa fedha 2016/17, jumla ya taasisi 416 kati ya 533, ziliwasilisha PPRA mipango ya manunuzi, na taasisi 237 ziliwasilisha tangazo la jumla la manunuzi kwa ajili ya kuchapishwa kwenye jarida la manunuzi na tovuti ya PPRA.

Aidha, PPRA ilichapisha taarifa za mikataba ya tenda 2,996 ukilinganisha na 1,977 kwa mwaka uliopita. Uchambuzi wa taarifa za mikataba hiyo umeainishwa katika **Jedwali namba 2-1:**

**Jedwali 2-1: Taarifa za mikataba**

| Na. | Makundi ya taasisi | Idadi ya mikataba iliyowasilishwa | Thamani (Shilingi milioni) |
|---|---|---|---|
| 1 | Halmashauri | 761 | 1,357,048 |
| 2 | Wizara | 225 | 28,566 |
| 3 | Mashirika ya umma | 845 | 260,972 |
| 4 | Wakala wa Serikali/ Mamlaka za maji | 301 | 121,322 |
| 5 | Idara zinazojitegemea | 841 | 3,149,158 |
| 6 | Ofisi za wakuu wa mikoa | 23 | 17,594 |
| | **Jumla** | **2,996** | **4,934,660** |

Uchambuzi wa taarifa za mikataba kulingana na aina ya manunuzi unaoneshwa kwenye **Jedwali 2-2:**

**Jedwali 2-2: Taarifa za mikataba na aina ya manunuzi**

| Na. | Aina ya manunuzi | Idadi ya taarifa za mikataba | Thamani ya mikataba (Shilingi Milioni) |
|---|---|---|---|
| 1 | Kazi za ujenzi | 1,028 | 3,676,089 |
| 2 | Bidhaa | 956 | 917,409 |
| 3 | Huduma za ushauri wa kitaalam | 234 | 198,538 |
| 4 | Huduma zisizohitaji ushauri wa kitaalam | 778 | 142,625 |
| | **Jumla** | 2,996 | 4,934,661 |

### 2.1.2 Ushirikiano na taasisi nyingine

Katika kutekeleza majukumu yake, PPRA inashirikiana na taasisi nyingine ili kuhakikisha manunuzi ya umma yanakuwa na tija kwa maendeleo ya nchi. Ushirikiano huu hutekelezwa kwa makubaliano maalum kati yake na taasisi hizo.

Katika mwaka wa fedha 2016/17, PPRA ilitekeleza makubaliano iliyoingia na bodi ya wataalam wa manunuzi (PSPTB) na Takukuru kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali 2- 3**

**Jedwali 2-3: Muhtasari wa utekelezaji wa makubaliano**

| Namba | Taasisi | Utekelezaji |
|---|---|---|
| 1 | PSPTB | • PPRA ilikagua sifa za wataalam wanaoshughulika na manunuzi kwenye taasisi.<br>• PPRA iliendesha mafunzo na kutoa vyeti ambavyo vinatambuliwa na PSPTB. |
| 2 | Takukuru | • Ripoti sita za ukaguzi ziliwasilishwa Takukuru kwa ajili ya uchunguzi kutokana na kukithiri kwa viashiria vya rushwa. Taasisi zilizohusika na ripoti hizo ni Makumbusho ya Taifa, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salam, DART, TCRA, Ofisi ya Bunge, na Wizara ya Maji.<br>• Ripoti 30 za ukaguzi maalumu wa miradi ya maji kutoka mamlaka 26 za serikali ziliwasilishwa Takukuru kwa uchunguzi<br>• Ripoti za miradi 21 kutoka taasisi tano zilizokaguliwa ziliwasilishwa Takukuru kwa uchunguzi. Taasisi hizo ni Manispaa ya Dodoma, Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge, Makumbusho ya Taifa, Wizara ya Maji na REA<br>• Ripoti za uchunguzi kutoka Taasisi ya Mifupa (MOI) na TCRA ziliwasilishwa Takukuru kwa uchunguzi zaidi. |

### 2.1.3 Kufungia wazabuni kushiriki kwenye zabuni za umma

PPRA imepewa mamlaka ya kufungia wazabuni kushiriki kwenye zabuni za umma kutokana na sababu mbalimbali, kama vile vitendo vya udanganyifu katika michakato au kukiouka masharti ya mikataba.


Katika mwaka wa fedha 2016/17, PPRA iliifungia kampuni ya Genuine Company Ltd, kwa muda wa mwaka mmoja.

### 2.1.4 Utoaji wa elimu

Katika mwaka wa fedha 2016/17, PPRA iliendelea kutoa elimu kwa makundi mbalimbali kuhusu sheria ya manunuzi ya umma kama ifuatavyo:

**a) Mafunzo**

Mafunzo maalum ya sheria ya manunuzi yalitolewa kwa watumishi 338 kutoka taasisi 17 za Serikali ikilinganishwa na watumishi 629 kutoka taasisi 29 waliopatiwa mafunzo hayo mwaka uliotangulia.




Pia, PPRA ilitoa mafunzo kwa wataalam 145 wa manunuzi na wa usimamizi wa fedha kutoka ofisi za wakuu wa mikoa na halmashauri zilizopo katika mikoa ya Dar es Salam, Mwanza, Tanga, Arusha, Dodoma, Morogoro, Mara na Manyara.

Aidha, PPRA ilitoa mafunzo ya sheria, kanuni na miongozo ya manunuzi ya umma kwa wataalam wa manunuzi 805 ukilinganisha na wataalam 205 katika mwaka uliotangulia.

Mwisho, PPRA ilitoa mafunzo kwa wajasiriamali wanawake 59 kuhusu fursa zilizopo kwenye manunuzi ya umma kwa makundi maalum. Mafunzo hayo yalihusisha wanawake wakandarasi, watoa huduma, washauri elekezi na wazabuni.




## b) Kongamano la Manunuzi ya Umma

Katika mwaka wa fedha 2016/17, PPRA iliandaa Kongamano la Mwaka la Manunuzi ya Umma ambapo wadau walijadili utekelezaji wa sheria ya manunuzi. Kongamano hilo lilihudhuriwa na washiriki 427 ukilinganisha na 430 wa mwaka uliotangulia. Kongamano hilo, lilijumuisha madiwani, wajumbe wa bodi za wakurugenzi za mashirika ya umma, watendaji wakuu na maafisa wengine wa serikali.

### c) Kongamano la Manunuzi ya Umma Afrika Mashariki

PPRA ilishiriki kwenye Kongamano la Tisa la Manunuzi ya Umma kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, lililofanyika Rwanda, Novemba 2016.

Kongamano hilo ni jukwaa linaloratibiwa na taasisi za usimamizi wa manunuzi ya umma kutoka nchi wanachama wa jumuiya hiyo kwa kupokezana, ambapo wadau mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi wanachama hushiriki.

### 2.1.5 Huduma za ushauri

Katika mwaka wa fedha 2016/17, PPRA ilitoa ushauri kwenye manunuzi ya dharura ambapo maombi 37 yalishughulikiwa.

### 2.1.6 Mfumo wa uwasilishaji na upokeaji taarifa kwa njia ya kielektroniki

PPRA iliendelea kuboresha mfumo wake wa uwasilishaji na upokeaji wa taarifa za manunuzi kwa njia ya kielektroniki ili kukidhi mahitaji ya kisheria. Aidha, maafisa 423 kutoka taasisi 237 walipatiwa mafunzo ya utumiaji wa mfumo huo.

### 2.1.7 Tovuti ya PPRA

Wadau wa manunuzi waliendelea kutumia tovuti www.ppra.go.tz ambapo watu hupata taarifa za manunuzi ikiwemo fursa za tenda, matangazo ya jumla ya tenda na matangazo ya mikataba ya tenda. Katika mwaka 2016/17, matangazo ya tenda 5,436 yalitangazwa kwenye tovuti.

### 2.1.8 Jukwaa la majadiliano mtandaoni

Jukwaa hili linawezesha wadau kujadiliana kuhusu manunuzi ya umma. Kwa mwaka wa fedha 2016/17, watumiaji 897 walisajiliwa, ikilinganishwa na watumiaji 844 kwa mwaka uliotangulia.

### 2.1.9 Huduma ya ujumbe mfupi wa simu

PPRA iliendelea kutumia huduma ya ujumbe mfupi wa simu ya kiganjani unaowawezesha wazabuni kupokea taarifa za tenda. Mzabuni anaweza kujiunga na huduma hii kwa kutuma ujumbe mfupi kwenda Namba **15332.** Katika mwaka 2016/17, idadi ya watumiaji iliongezeka kufikia 1,430 ikilinganishwa na 1,393 mwaka uliotangulia.




### 2.1.10 Mfumo wa manunuzi kwa njia ya mtandao

Kwa mwaka 2016/17, PPRA iliendelea na maandalizi ya mfumo wa manunuzi kwa njia ya mtandao ikiwa ni pamoja na kuwaelimisha wadau na kufanya majaribio ya matumizi ya mfumo huo.

## 2.2 PPRA katika kufikisha huduma kwa wadau

Katika mwaka wa fedha 2016/17, PPRA iliendelea kutekeleza sera na mkakati wa mawasiliano katika utoaji wa taarifa za manunuzi ya umma kwa wadau wake kama ifuatavyo:

### *a) Tuzo ya umahiri wa uandishi wa habari za manunuzi*


Ili kuongeza uelewa wa wadau kuhusu manunuzi ya umma, PPRA iliendelea kushirikiana na Baraza la Habari Tanzania kwa kudhamini tuzo ya mwandishi bora wa mwaka.

### *b) Tanzania Procurement Journal*

Jarida la *Tanzania Procurement Journal* hutumiwa na wadau wa manunuzi kama kituo cha taarifa zote za manunuzi ya umma. Katika mwaka wa fedha 2016/17, PPRA iliandaa matoleo 52 na kuchapisha nakala 780,000 zikiwa na taarifa za tenda na matangazo mbalimbali pamoja na ripoti za ukaguzi wa manunuzi. Nakala hizi husambazwa kila siku ya Jumanne kupitia gazeti la *Daily News*.

### c) *Vipindi vya elimu kwa umma*

PPRA ilirusha matangazo ya redio na televisheni kuhusu uadilifu na madhara ya rushwa kwenye manunuzi ya umma. Aidha, PPRA ilichapisha toleo la wananchi la ripoti ya tathmini ya utendaji ya mwaka wa fedha 2015/16 na tafsiri ya toleo la wananchi kwa lugha ya Kiingereza.




## 2.3 Kuboresha mazingira ya kazi na maslahi ya watumishi wa PPRA

PPRA iliendelea kuboresha mazingira ya kazi, mifumo na vitendea kazi kwa ajili ya kuongeza motisha kwa wafanyakazi ili waweze kufikia malengo ya taasisi.

## SURA YA TATU

### 3.0 Ukaguzi wa manunuzi ya umma

### 3.1 Idadi ya mikataba ya manunuzi

Katika mwaka wa fedha 2016/17, taasisi 186 kati ya 533, sawa na asilimia 35 ziliwasilisha taarifa za mikataba yao PPRA. Kiwango cha uwasilishaji wa taarifa hizo kilipungua ikilinganishwa na mwaka uliotangulia ambapo taasisi 322 kati ya 493, sawa na asilimia 65, ziliwasilisha. Uchambuzi wa idadi ya mikataba iliyowasilishwa umeainishwa kwenye **Jedwali 3-1.**

**Jedwali 3-1: Uchambuzi wa idadi na aina ya mikataba**

| Na. | Aina za mikataba | Idadi ya mikataba | Thamani ya mikataba (Bilioni) | Asilimia ya jumla ya tuzo za mikataba |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Bidhaa | 51,028 | 1,058.87 | 16.8 |
| 2. | Kazi za ujenzi | 3,638 | 4,743.60 | 75.2 |
| 3. | Huduma za ushauri wa kitaalam | 598 | 256.69 | 4.1 |
| 4. | Huduma zisizohitaji ushauri wa kitaalam | 17,885 | 251.79 | 4.0 |
| 5. | Uuzaji wa mali za Serikali kwa njia ya tenda | 5 | 0.10 | 0.0 |
| | **Jumla** | **73,154** | **6,311.05** | **100.0%** |

### 3.2 Thamani ya mikataba ya manunuzi

Uchambuzi wa taarifa kuhusu thamani ya mikataba unaonesha taswira halisi ya manunuzi ya serikali kwani taasisi 23 zilizofanya manunuzi makubwa yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 20 kwa kila taasisi, zilikuwa miongoni mwa zile zilizowasilisha taarifa.

Mikataba iliyotolewa na taasisi hizo kwa mwaka wa fedha 2016/17, ilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 5,697 sawa na asilimia 90 ya thamani ya mikataba ya taasisi 186 zilizowasilisha taarifa za mikataba ya tenda. Uchambuzi zaidi wa taarifa za mikataba unaoneshwa kwenye **Jedwali 3-2.**

**Jedwali 3-2: Mchanganuo wa tuzo za mikataba ya manunuzi**

| Mwaka wa fedha | Idadi ya taasisi ambazo taarifa za mikataba yake zilipokewa | Idadi ya taarifa za mikataba zilizopokewa | Thamani ya mikataba iliyopokewa (Shilingi bilioni) | Jumla ya bajeti (Shilingi bilioni) |
|---|---|---|---|---|
| 2013/14 | 235 | 74,208 | 4,859 | 18,249 |
| 2014/15 | 267 | 75,509 | 4,349 | 19,853 |
| 2015/16 | 322 | 109,575 | 3,001 | 22,495.5 |
| 2016/17 | 186 | 73,154 | 6,310 | 20,696 |

Mikataba 19,456 ilikuwa kwa njia ya manunuzi madogomadogo; mikataba 12,095 ilikuwa ya njia ya ushindani mdogo; na mikataba 17,706 iliingiwa ya njia nyinginezo.

### 3.2.1 Uwiano wa bajeti na manunuzi

Uchambuzi wa taarifa za bajeti zilizowasilishwa na taasisi za Serikali 186 unaonesha kuwa kiasi cha shilingi bilioni 20,696 kilipokewa au kukusanywa ambacho ni sawa na asilimia 81.77 ya bajeti zao ambayo ni shilingi bilioni 25,311. Aidha, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa asilimia 31.71 ya fedha zilizopokewa au kukusanywa, zilitumika kwenye manunuzi.

Katika mwaka husika, kiwango cha fedha kilichotumika kwenye manunuzi dhidi ya mapato yaliyokusanywa kilishuka kwa asilimia tano ikilinganishwa na asilimia 37 kwa mwaka uliotangulia.

### 3.2.2 Mgawanyiko wa jumla ya thamani ya mikataba

Mgawanyiko wa thamani ya mikataba kwa taasisi 186 unaonesha kwamba katika shilingi bilioni 6,310 zilizotumika kwenye manunuzi, asilimia 75 ilitumika kwenye miradi ya kazi za ujenzi, asilimia 17 kwenye manunuzi ya bidhaa, asilimia nne kwenye huduma za ushauri wa kitaalam, asilimia nne huduma zisizohitaji ushauri wa kitaalam na asilimia 0.002 zilipatikana kutokana na uuzaji wa mali za umma kwa njia ya tenda.

Jumla ya thamani ya manunuzi yaliyofanywa na Rahco, Tanroads, MSD na Tanesco ilikuwa shilingi bilioni 4,651. Sehemu kubwa ya manunuzi ilikuwa ya kazi za ujenzi zilizofanywa na Rahco na Tanroads ikifuatiwa na manunuzi ya bidhaa yaliyofanywa na MSD.

### 3.2.3 Thamani ya mikataba kulingana na makundi ya taasisi

Mchanganuo wa jumla ya fedha iliyotumika kwenye manunuzi katika asilimia ni kama ifuatavyo:

i) Mashirika ya umma, asilimia 59;
ii) Wakala wa serikali na mamlaka za maji, asilimia 30;
iii) Wizara, asilimia 2.4;
iv) Halmashauri, asilimia 4.3;
v) Idara zinazojitegemea, asilimia 3.9; na
vi) Ofisi za wakuu wa mikoa, asilimia 0.3.

## 3.3 Matokeo ya ukaguzi wa manunuzi


### 3.3.1 Malengo ya ukaguzi

Sheria ya manunuzi ya umma imeipa PPRA mamlaka ya kufanya ukaguzi wa manunuzi yanayofanywa na taasisi za Serikali kuanzia wakati wa mchakato wa tenda, utekelezaji wa mikataba na baada ya kukamilika kwa mikataba.

Malengo ya ukaguzi, pamoja na mambo mengine, ni kuangalia iwapo manunuzi yalizingatia sheria, taratibu na iwapo miradi iliyotekelezwa ilileta matokeo yaliyokusudiwa.

PPRA ilifanya ukaguzi wa uzingatiaji wa sheria ya manunuzi, na uhakiki kwa taasisi 112 zikiwemo taasisi 43 zilizopo kwenye kundi la wizara, idara zinazojitegemea na wakala wa serikali; halmashauri 35 na mashirika ya umma 34. Aidha, taasisi 81 kati ya hizo, zilifanyiwa ukaguzi wa kupima thamani ya fedha kwenye miradi.

Ukaguzi uliofanywa ulihusu manunuzi ya taasisi za Serikali katika mwaka wa fedha 2016/17, na pia ulipima utekelezaji wa mapendekezo ya PPRA ya mwaka wa fedha 2015/16. Aidha, taasisi nane zilifanyiwa uchunguzi kubaini ukiukwaji wa sheria na taratibu.




### 3.3.2 Uchaguzi wa taasisi na maeneo ya ukaguzi

Uchaguzi wa taasisi kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi ulizingatia uwepo wa vihatarishi. Taasisi ambazo jumla ya thamani ya manunuzi yake ilizidi shilingi bilioni 20 zilijumuishwa moja kwa moja kwenye ukaguzi; wakati taasisi nyingine zilichaguliwa kwa kuzingatia kigezo kimoja au zaidi kati ya vifuatavyo:

- i) Taasisi zilizoripotiwa kuhusiana na ukiukwaji wa sheria au taratibu za manunuzi;
- ii) Taasisi zilizokuwa na tuhuma zilizosababisha kufanyiwa uchunguzi na PPRA;
- iii) Taasisi zilizopata maksi za chini katika ukaguzi uliopita;
- iv) Taasisi ambazo hazikuwa zimekaguliwa kwa muda mrefu; na
- v) Taasisi zilizopo maeneo jirani na ukaguzi.

### 3.3.3 Aina za ukaguzi zilizofanywa

#### *a) Ukaguzi wa uzingatiaji wa sheria*

Ukaguzi huu ulilenga kupima iwapo michakato ya tenda ilizingatia sheria ya manunuzi. Aidha, ukaguzi uliangalia tenda yenye gharama kubwa pamoja na zile zalizokuwa na uwezekano wa kupotea kwa fedha za umma.

### b) *Ukaguzi wa kupima thamani ya fedha kwenye miradi*

Ukaguzi huu ulilenga miradi iliyotekelezwa kwa kuangalia utekelezaji wa mikataba ya bidhaa, kazi za ujenzi na huduma za ushauri wa kitaalam. Aidha, ukaguzi uliangalia njia zilizotumika kuendesha tenda, iwapo mkataba wa tenda ulisainiwa mpaka kufikia mwaka wa fedha 2016/17, thamani ya mikataba iliyoingiwa na iwapo mradi ulikuwa wa barabara, madaraja, majengo, miradi ya maji, pamoja na vifaa.
**Jedwali 3-3** linaonesha aina ya tenda, idadi na thamani.


**Jedwali 3-3: Tenda zilizokaguliwa**

| Na | Tenda | Idadi ya tenda | Thamani ya tenda (shilingi bilioni) |
|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi | 1,028 | 3.68 |
| 2 | Vifaa | 956 | 917.41 |
| 3 | Kazi za ushauri wa kitaalam | 234 | 198.54 |
| 4 | Kazi zisizohitaji ushauri wa kitaalam | 778 | 142.63 |
| | **Jumla** | **2,996** | **1,262.26** |

### c) *Udanganyifu na rushwa kwenye manunuzi ya umma*

Masuala ya udanganyifu na rushwa katika manunuzi ya umma yalifuatiliwa kwa kuzingatia makubaliano kati ya PPRA na Takukuru. Katika makubaliano hayo, viashiria kadhaa vya rushwa vimeainishwa ambavyo PPRA huvitumia katika ukaguzi wake. Viashiria hivyo vikiwa vingi ni ishara ya uwezekano wa kuwapo kwa vitendo vya rushwa na udanganyifu kwenye tenda husika.

Ni muhimu kutambua kwamba uwepo wa viashiria vya rushwa kwenye manunuzi siyo ushahidi pekee wa rushwa kwenye tenda. Hata hivyo, viashiria hivyo vinapokuwa vingi, PPRA hupeleka Takukuru ripoti ya ukaguzi ya taasisi husika kwa uchunguzi zaidi.




### *3.3.4 Matokeo ya ukaguzi wa uzingatiaji wa sheria*

Wastani wa jumla wa uzingatiaji wa sheria ya manunuzi kwa taasisi zilizokaguliwa ni maksi 74, kiwango ambacho ni cha juu ikilinganishwa na maksi 73 kwa mwaka uliopita. Hata hivyo, wastani huo ulikuwa chini ya lengo lililowekwa, yaani maksi 80.

Uchambuzi unaonesha kwamba taasisi 10 kati ya 112 zilipata kiwango kisichoridhisha yaani chini ya maksi 60, katika uzingatiaji wa sheria. Taasisi 68 zilipata kiwango cha kati, yaani maksi 61 hadi 79 na taasisi 34 zilipata kiwango cha kuridhisha, yaani maksi 80 na zaidi. Taasisi zilizopata maksi zisizoridhisha ni pamoja na Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela, soko la Kariakoo, TTCL, Mamlaka ya Maji Lindi, na halmashauri za wilaya za Pangani, Kahama, Kibondo, Kasulu, Masasi na Handeni.

Vigezo vilivyotumika kupima uzingatiaji wa sheria vilikuwa saba ambavyo ni:

i) Muundo wa uendeshaji manunuzi kitaasisi;
ii) Uandaaji na utekelezaji wa mpango wa manunuzi;
iii) Uendeshaji wa michakato ya tenda;
iv) Usimamizi wa mikataba;
v) Utunzaji wa nyaraka za tenda;
vi) Utumiaji wa mifumo ya PPRA; na
vii) Ushughulikiaji wa malalamiko ya wazabuni.

Wastani wa uzingatiaji wa sheria unaonesha kuwa taasisi zilifanya vizuri kwenye maeneo mawili ambayo ni; muundo wa uendeshaji wa manunuzi kitaasisi ambapo zilipata maksi 80 na katika usahihi wa michakato ya tenda maksi 82.

**Jedwali 3-4: Wastani wa uzingatiaji wa sheria**

| Na. | Muundo wa uendeshaji wa manunuzi kitaasisi | Maksi | Wastani |
|---|---|---|---|
| 1 | Uandaaji na utekelezaji wa mpango wa manunuzi | 80 | Kuridhisha |
| 2 | Usahihi katika michakato ya tenda | 78 | Kati |
| 3 | Usimamizi katika utekelezaji wa mikataba | 76 | Kuridhisha |
| 4 | Utunzaji wa kumbukumbu za manunuzi | 68 | Kati |
| 5 | Utumiaji wa mifumo ya PPRA | 48 | Kutoridhisha |
| 6 | Ushughulikiaji wa malalamiko ya Wazabuni | 10 | Kutoridhisha |
| | | | |

Katika taasisi 112 zilizokaguliwa, 10 zilikatwa maksi kwa kutoshughulikia malalamiko ipasavyo. Taasisi hizo ni Necta, Tanesco, MOI, Tanroads – Arusha, IAA, AICC, Chuo cha Kumbukumbu cha Mwalimu Nyerere, Halmashauri ya Wilaya ya Meru, TTCL na Soko la Kariakoo.

### 3.3.5 Matokeo ya ukaguzi wa kupima thamani ya fedha


Wastani wa jumla wa kupima thamani halisi ya fedha kwa taasisi 81 zilizokaguliwa ni maksi 82.5, kiwango ambacho ni cha kuridhisha.

Vigezo vitano vilivyotumika katika kupima kama thamani halisi ya fedha ilipatikana kwenye miradi ya ujenzi ni kama inavyoonyeshwa kwenye **Jedwali 3-5.**

**Jedwali 3-5: Vigezo vya kupima thamani ya fedha**

| Na. | Muundo wa uendeshaji wa manunuzi kitaasisi | Maksi | Wastani |
|---|---|---|---|
| 1 | Uandaaji, usanifu na utunzaji wa nyaraka za tenda | 85 | Kuridhisha |
| 2 | Mchakato wa tenda | 81.5 | kuridhisha |
| 3 | Usimamizi wa utekelezaji miradi ya ujenzi | 75.6 | Kawaida |
| 4 | Ubora na ukubwa wa miradi ya ujenzi iliyotekelezwa | 85.9 | Kuridhisha |
| 5 | Ufungaji wa miradi | 68.2 | Kawaida |

Aidha, uchambuzi ulionyesha kuwa miradi 10 kati ya 210 iliyokaguliwa, ilifanya vibaya




### 3.4 Ukaguzi wa viashiria vya rushwa

#### 3.4.1 *Matokeo ya ukaguzi wa viashiria vya rushwa*

Kati ya taasisi 112 zilizokaguliwa, taasisi 17 zilibainika kuwa na viashiria vya rushwa ambapo taasisi ya Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela kiliongoza kundi hili.

#### *3.4.2 Matokeo ya tathmini ya viashiria vya rushwa kwenye miradi*

Ukaguzi uliofanywa na PPRA pia ulipima uwezekano wa uwepo wa rushwa katika taasisi au miradi husika. Tathmini ya jumla ya viashiria vya rushwa inaonesha kwamba taasisi 17 na miradi 34 vilibainika kuwa na kiwango kikubwa cha viashiria vya rushwa ikimaanisha kuwepo kwa uwezekano mkubwa wa uwepo wa vitendo vya rushwa katika taasisi na miradi hiyo.

Taasisi hizo ni mamlaka za maji safi na maji taka za Moshi (Muwasa), Mwanza (Mwauwasa) na Arusha (Auwasa); pamoja na Halmashauri za wilaya za Msalala, Kibondo na Moshi. Taasisi nyingine ni Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela, Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Chuo cha Ufundi Arusha, Halmashauri ya Mji wa Kahama, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Taasisi ya Uhasibu Arusha (IAA),

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, TRA, Halmashauri ya Mji wa Masasi, pamoja na Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC).

### *3.4.3 Malipo yenye utata*

Katika mwaka wa fedha 2016/17, ukaguzi ulibaini malipo yenye utata yaliyofanywa na taasisi tatu kwenye miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 3.09, ambapo jumla ya shilingi milioni 483.44 au asilimia 15.6, zililipwa kwa wakandarasi kwa kazi ambazo hazikuwa zimefanywa. Taasisi hizo ni Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba, NSSF na TTCL.

## 3.5 Uchunguzi wa ukiukwaji wa sheria

Katika mwaka wa fedha 2016/17, PPRA ilifanya uchunguzi wa tuhuma nane zilizohusu mikataba 10 ya manunuzi inayokadiriwa kuwa na thamani ya shilingi bilioni 280. Uchunguzi huo uliozihusu taasisi nane ulitokana na maagizo ya viongozi wa Serikali au taarifa zilizopokewa kutoka vyanzo mbalimbali kama vile vyombo vya habari, taasisi za Serikali na wananchi.

Kwa ujumla, Serikali iliweza kuokoa shilingi bilioni 42.97 kutokana na uchunguzi huo baada ya PPRA kuingilia kati na kusimamisha michakato wa tenda tatu kwa kuwa Serikali isingepata thamani bora ya fedha kwenye tenda hizo.

Pia, uchunguzi huo ulibaini kuwa Serikali ingeweza kuokoa takriban shilingi bilioni 1.62 kama taasisi zilizochunguzwa zingekuwa zimetekeleza mapendekezo yaliyotolewa na PPRA.

## SURA YA NNE

## 4.0 Changamoto na ufumbuzi wake

### 4.1 Changamoto

Kwa mwaka wa fedha 2016/17, kulikuwa na changamoto za kisekta na za ndani ya PPRA kama ifuatavyo:

#### 4.1.1 Changamoto za kisekta

a) Baadhi ya taasisi kutowasilisha PPRA, ripoti na taarifa mbalimbali za tenda kwa wakati, hivyo kuikwamisha katika kutekeleza majukumu yake;

b) Ukosefu wa muunganiko baina ya mfumo wa manunuzi kwa njia ya kieletroniki na mifumo mingine ya Serikali, hivyo kuathiri utekelezaji wa mfumo huo;

c) Baadhi ya taasisi za Serikali kutosimamia ipasavyo utekelezaji wa mikataba ya manunuzi, na hivyo kukwamisha upatikanaji wa thamani bora ya fedha.

d) Kukosekana kwa msawazisho wa bidhaa na huduma zinazotumiwa Serikalini, hivyo kusababisha tofauti ya bei na ubora kwa bidhaa na huduma za aina moja;

e) Tofauti katika baadhi ya taratibu za tenda zinazotumiwa na halmashauri na zile za taasisi nyingine za Serikali, hivyo kuleta mgongano wa maslahi na ukiukwaji wa taratibu za tenda;

f) Kiwango cha chini cha weledi na kukosekana kwa uadilifu miongoni mwa watumishi wa umma na wazabuni na hivyo kuzuia upatikanaji wa thamani bora ya fedha;

g) Uhaba wa watumishi katika taasisi zinazoshughulikia masuala ya manunuzi ya umma kuanzia ngazi ya usimamizi hadi utekelezaji, hivyo kuathiri utendaji wa taasisi husika;

h) Ufanisi mdogo kwa baadhi ya taasisi za Serikali katika kuendesha mchakato wa tenda na hivyo kusababisha ongezeko la gharama na muda katika utekelezaji wa miradi;

i) Baadhi ya watumishi wa umma na wazabuni kutokuwa na uelewa wa kutosha wa sheria ya manunuzi ya umma, hivyo kushindwa kufanya uamuzi sahihi katika michakato;

j) Matumizi yasiyoridhisha ya mifumo ya PPRA, hivyo kuathiri ufuatiliaji wa shughuli za manunuzi ya taasisi husika;




### 4.1.2 Changamoto za ndani ya PPRA

a) Uhaba wa rasilimali watu na fedha, hivyo kuathiri utekelezaji wa mpango mkakati wake;
b) Ukosefu wa jengo la ofisi na hivyo kusababisha gharama kubwa za uendeshaji kutokana na malipo ya kodi ya pango; na
**c)** Kutokidhi stahiki za watumishi wake kwa wakati, hivyo kuathiri morali ya watumishi.

### 4.1.3 Ufumbuzi

Katika kukabiliana na changamoto zilizoainishwa, PPRA itachukua hatua zifuatazo:

a) Itaendelea kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa sheria ya manunuzi ya umma;
b) Itaendelea kutoa elimu kwa taasisi za Serikali na wadau wengine kuhusu sheria ya manunuzi na juu ya hatua za kuchukua dhidi ya ukiukwaji wa sheria;
c) Itashirikiana na wadau wa mifumo mingine ya Serikali ili kuunganisha mfumo wa manunuzi kwa njia ya kieletroniki na mifumo hiyo;
d) Itashirikiana na taasisi zenye jukumu la kuandaa na kuhakiki ubora wa bidhaa na huduma zinazotumiwa na taasisi za Serikali; na
e) Itaanzisha wiki ya manunuzi ya umma kwa ajili ya kuitangaza PPRA na kutoa taarifa mbalimbali za manunuzi kwa umma.

Kwa upande wa changamoto za ndani, PPRA itaimarisha upatikanaji na ukusanyaji wa fedha na itaendelea kutangaza shughuli zake, ili kuongeza vyanzo vya fedha.